

## **TAARIFA ZA MAENDELEO YA KATA ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA 2018/19**

### **MAMLAKA YA MJI MDOGO WA MWANGA**

Mheshimiwa Diwani wa Mwanga aliwasilisha taarifa. Alieleza kwamba vikao vyote vya kisheria vilifanyika na hali ya ulinzi ni salama na matukio machache yaliyojitokeza ya uhalifu yalikabiliwa na vyombo vya dola. Alieleza kuwa Mikutano Mikuu na vikao vya kisheria vilifanyika.

Aidha, shughuli za utekelezaji zinazoendelea ni; Mamlaka ya Maji Mwanga ilizalisha maji kiasi cha mita za ujazo 144, 156 na deni la maji hadi sasa ni Sh. 223, 376, 914.08.

Alieleza kuna mradi wa madarasa 2 na Ofisi 1 na darasa hilo limefikia hatua ya kupauliwa ambapo mradi huo unaghanimu Sh. 42,233,280.00. Pia, kuna ukamilishaji wa milango na madirisha shule ya Sekondari AshaRose Migiro.

Kwa upande wa Afya huduma ya chanjo ilitolewa kwenye Kituo cha Mwanga na Neema. Makusanyo ya mfuko wa afya ya jamii (iCHF) ni Sh. 135,000.27 na Papo kwa papo iliyokusanya jumla ya Sh.6,058,000.00. Aidha, wanachama waliojiunga iCHF ni 51.

Kwa upande wa ukaguzi wa majengo ya biashara sehemu mbalimbali zilikaguliwa. Pia, wafugaji waliopewa ushauri ni 632, matibabu kwa mifugo ilitolewa na wafugaji walielimishwa namna ya kuepuka magonjwa.

Alieleza kuwa wakulima 219 walipewa ushauri hasa wakulima na walishauriwa kupanda mazao yanayostahimili ukame.

Alieleza uhifadhi wa Mazingira umepewa kipaumbele ikiwa ni pamoja na kuimarisha usafi wa mji kwa kufanya usafi wa kila mwisho wa mwezi.

Aidha, Mamlaka ya Mji Mdogo Mwanga ilikusanya jumla ya Sh. 39,055,002.45 katika vyanzo vyake vya ndani vya mapato.

### **KATA YA NGUJINI**

Mheshimiwa Diwani, ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri aliwasilisha taarifa. Alieleza kwamba suala la ulinzi na usalama unaridhisha na uhusianao baina ya wafugaji na wakulima ni mzuri.

Aidha, vikao vya kisheria vilifanyika. Alieleza migogoro ya ardhi na uhamiaji haramu hakuna na uhusiano wa wakulima na wafugaji ni mzuri.

Alieleza kuwa shughuli zilizofanyika kwa upande elimu ni ufundishaji mashulen, mitihani ya darasa la saba ilifanyika, upokeaji wa ruzuku toka Serikalini, uundwaji wa kamati za kudhibiti ubora wa elimu kwa kila shule, udhibiti wa kitaaluma wa mara kwa mara, vikao kazi vya wakuu

wa shule na walimu, ufuatiliaji wa mahudhurio ya walimu na wanafunzi na uwasilishaji wa taarifa mbalimbali za elimu Wilayani.

Pia, kwa sekta ya kilimo na ufugaji ushauri wa kitaalaam ultolewa kwa wakulima na wafugaji na ukaguzi wa nyama kabla ya kuuza kwa waliji ulifanyika.

Kwa upande wa Afya, huduma ya kliniki ya wajawazito na watoto na chanjo na elimu ya afya iliendelea kutolewa katikajamii. Pia, uchangiaji wa iCHF, NHIF na Papo kwa papo ni Sh. 3,797,184.22 na salio anzia ilikuwa ni Sh.3,189,999.22 kwenye Zahanati ya Ngujini na Zahanati ya Songoa.

Alieleza kuwa taarifa ya mapato na matumizi zilisomwa kwenye mikutano mikuu ya vijiji ambapo alifafanua kuwa mapato ya Halmashauri ya Vijiji vya Ngujini, Chanjale na Songoa ni Sh. 2,399,400.00, alieleza katika fedha za TASAF kwa walengwa ziliwafikia. Kwa Halmashauri ya Wilaya ilikusanya jumla ya Sh. 144,600.00. Pia, kuna fedha zilizotolewa kwa ajili ya miradi ya TASAF III ambayo ni Sh.2,368,000.00.

### **KATA YA MSANGENI**

Mheshimiwa Diwani aliwasilisha taarifa. Alieleza kuwa hali ya ulinzi na usalama ilikuwa shwari kiasi, kwa sababu upande wa mali za wananchi ultokea wizi na watuhumiwa walikamatwa na hatua za kisheria zilichukuliwa.Pia, vikao vya kisheria vilifanyika.

Shughuli zilizofanyika za mifugo ni matibabu, upigaji chapa ng'ombe, ukaguzi wanyama, ukataji wa pembe na ushauri nasaha ultolewa kwa wafugaji. Pia, wakulima walipatiwa ushauri kuhusu kilimo bora, uhamasishaji wa mazao ya biashara na takwimu za wakulima wote zilikusanywa kwa ajili ya ufuatiliaji.

Aidha, upande wa mazingira, usafi wa kila mwisho wa mwezi unaendelea kufanyika. Pia wananchi wamehamasishwa kuacha kupanda miti ya Acrocarpus na Eucalyptus katikavyanzo vya maji

Alieleza kwa upande wa elimu, udhibiti wa utoro na mimba kwa wanafunzi ulisimamiwa vizuri, chakula cha mchana bado kuna baadhi ya wazazi hawaajaanza kuwalipia watoto wao chakula ila uhamasishaji kwa wazazi unaendelea na vikao vya wazazi vilifanyika.

Pia, shughuli za ujenzi na ukarabati unaendeleakatika Zahanati ya Sungo na kuna ukamilishaji wa choo kipy. Alieleza kijiji cha Mamba kinatekeleza ujenzi wa choo na uhamasishaji wa michango kwa wananchi unaendelea. Kuna ujenzi wa choo na wananchi wamechangia katika Zahanati ya Kyanga ambapo kwa sasa kimeanza kutumika. Alifafanua kuwa ujenzi mwengine wa choo kijiji cha Simbomu unatekelezwa kwa nguvu za wananchi na hatua iliyofikiwa ni ukamilishaji wa msingi.

Miradi ya maji inaendelea kutoa huduma kwa wananchi kwa usimamizi wa Jumuiya za Watumia maji zilizopo vijiji vya Msangeni na Mamba. Mkandarasi ameshaanza kazi ya uchimbaji katika Kijiji cha Mruma na kuna uhaba wa maji katika vijiji vya Mwai na Simbomu.

Alieleza kuwa kijiji cha Msangeni kimekarabati barabara kupitia nguvu za wananchi yaani msaragambo ambazo zilikuwa zimeharibiwa na mvua za masika. Pia greda lilichimba barabara na kurekebisha sehemu korofi kwenye baadhi ya barabara katika kijiji cha Msangeni. Uchimbaji wa barabara 2 ulifanywa chini ya usimamizi wa TARURA

Pia, mfuko wa afya ya jamii iliyoboreshwa iCHF unaendelea kuhamasishwa na wananchi kwa kata nzima na makusanyo ya iCHF ni Sh. 420,000.00 na Papo kwa papo ni Sh. 174,000.00. Alieleza Halmashauri ya Wilaya imekusanya mapato Sh. 599,000.00 na mapato ya Vijiji ni Sh. 134,000.00.

### **KATA YA KIGONIGONI**

Mheshimiwa Diwani aliwasilisha taarifa na alieleza kwamba hali ya ulinzi na usalama haikuwa nzuri, kwa sababu mvuvi mmoja alijeruhija vibaya na Kiboko, uvamizi wa makundi ya Tembo na ajali mbaya ya pikipiki iliyosababisha mtu kupoteza maisha. Alieleza kuwa vikao vya kisheria vilifanyika.

Vilevile mazao na miche yamesombwa na mvua, na ugonjwa wa fungasi uliathiri mazao japo hali ya chakula ni nzuri. Alieleza zoezi la ukataji wa leseni limeteklezwa vizuri baada ya Kamati ya fedha, uongozi na mipango kufanya ziara Ziwa Jipe.

Kwa upande wa Elimu, Idara ya Elimu Msingi na Sekondari zote zina upungufu wa walimu. Katika Shule ya Sekondari Kigonigoni kuna mradi mpya wa maji na mradi wa bweni la wanafunzi. Uogozi wa shule kwa kushirikiana na wazazi wamefanikiwa kuchoma matofali 9,000.

Shukrani zimetolewa kwa Serikali kuwapatia mradi wa ujenzi wa darasa 1 wenye thamani ya Sh. 17,843,824.86 na umekamilika na kupatiwa walimu wa Sanaa japo kuna upungufu wa walimu wa Sayansi.

Kwa elimu Msingi mradi wa choo cha wanafunzi unaendelea na mradi wa maji unaendelea vizuri na shule ya Msingi Kwakihindi mradi wa nyumba ya mwalimu unaendelea vizuri. Alifafanua kuwa, kuna ukarabati wa nyumba ya mwalimu shule ya msingi Kigonigoni na unaendelea vizuri japo kuna upungufu wa fedha Sh. 4,092,000.00 ili kukamilisha mradi huo.

Mradi wa kivuko cha shambani cha Kwakitia unaendelea vizuri na wananchi wanaomba fedha ili kukamilisha ujenzi wa kivuko hicho.

Alifafanua kuwa, kuna mradi wa majengo mapya Kituo cha Afya Kigonigoni na unaendelea vizuri na wataalam mbalimbali wapo katika kutatua changamoto zilizopo. Kwa upande wa afya hakuna magonjwa ya milipuko, dawa muhimu zilipatikana na uhamasishaji wa kijiungu na iCHF unaendelea. Alieleza waliojiunga na iCHF ni 18 na fedha iliyokusanya ni Sh. 1,080,000.00 na makusanyo ya papo kwa papo ni Sh. 416,000.00.

Aidha Mapato ya Halmashauri ya Vijiji yaliyokusanya jumla ni Sh. 655,000.00 na mapato ya Halmashauri ya Wilaya ni Sh. 20,000.00.

### **KATA YA KWAKOA**

Mheshimiwa Diwani aliwasilisha taarifa. Alieleza kwamba hali ya ulinzi na usalama ilikuwa ni nzuri. Pia, kulikuwa na mgawanyiko kwenye Serikali ya Kijiji japokuwa kwa sasa mgogoro umeshatatuliwana shughuli za maendeleo kijijini zinaendelea vizuri. Aidha, vikao vya kisheria zikiwemo Halmashauri za Vijiji na mikutano mikuu ilifanyika baadhi. Alieleza kwa upande wa Afya, Zahanati ya Kwakoa inahitaji ukarabati mkubwa kwa sababu kuna uchakavu wa sakafu, siling bodi na madirisha.

Alieleza kwa upande wa Kilimo, hali ya chakula ni ya wastani na kuna uharibifu wa mazao uliofanywa na Tembo na Nyati. Mvua zilinyesha za kutosha na wadudu waharibifu wa mazao walijitokeza maeneo mengi ya Kata. Hali yamazao mashambani ni nzuri na kuna matarajio makubwa ya kupata mavuno ya kutosha.

Aidha, alieleza kwa upande wa Elimu Sekondari, kuna ujenzi wa bweni la wavulana Kwangu sekondari. Alieleza kuna ujenzi wa shule ya msingi Mgigili na shule ya sekondari Kwangu madarasa ni mabovu na Halmashauri imeombwa kuchangia fedha za ukarabati.

### **KATA YA JIPE**

Mheshimiwa Diwani aliwasilisha taarifa. Alieleza kwamba hali ya ulinzi na usalama ni shwari. Alifafanua kuwa suala la uhamiaji haramu haukujitokeza na uhusiano bainaya wafugaji na wakulima ni mzuri. Alieleza usafi kuwa, suala la usafi wa mazingira kila mwisho wa mwezi linatekelezwa. Alieleza kuwa vikao vya kisheria vilifanyika baadhi.

Kwa upande wa maendeleo ya jamii, idara ya maendeleo ya jamii imetoa huduma ya mikopokwa vijiji vya Butu na Jipe. Kwa upande miundombinu, kwa kipindi cha mvua barabara ziliharibika na Serikali ilifanyamarekebisho kwa baadhi ya sehemu. Pia, Serikali inapongezwa kwa kuweka umeme Kijiji cha Butu naKambi ya Simba, mkandarasi anaendelea na zoezi la kufunga nyaya za umeme. Aidha, kwa upande wa kilimo, mvua bado zilikuwa hazijanyesha na wakulima walikuwa kwenye maandalizi. Vilevile, alieleza kuwa uchomaji wa mkaa umepungua kidogo kwa sababu wananchi wengi wamepata mazao na wameacha zoezi la uchomaji wa mkaa.

Aidha, elimu msingi shughuli iliyotekelawa ni ufundishaji, chakula cha mchana wanafunzi walipatiwa. Alieleza elimu sekondari, maji ni kidogo sana kwenye sekondari ya Jipe na jitihada zinatakiwa zifanyike ili yaweze kukidhi mahitaji. Alieleza kuwa, Kata ya Jipe imekusanya michango ya iCHF jumla ya Sh. 630,000.00 na Papo kwa Papo imekusanya Sh. 1,140,093.00. Kwa upande wa mapato ya Halmashauri ya Kijiji jumla zimekusanya Sh. 700,800.00. Vilevile kwa upande wa mifugo, malisho yalikuwepo ya kutosha japo kuwa ugonjwa wa homa ya mapafuambao uliathiri mifugo. Alieleza, uvuvi wa samaki wakubwa wanapatikana, hivyo inapunguza uvuvi haramu wa kuvua samaki wadogo.

## KATA YA SHIGHATINI

Mheshimiwa Diwani aliwasilisha taarifa. Alifafanua kuwa hali ya ulinzi na usalama haikuwa salama kwa sababu nyaraka za ofisi zilipotea kutoptana na ofisi kuungua. Fedha za ukarabati wa ofisi hiyo ziliombwa lakini hazijatolewa.

Vilevile, alieleza kuwa ipo migogoro ya ardhi hasa kwenye mipaka ya Vijiji ambavyo ni Vuchama Ndambwe, Shighatini na Ibaya, hali inayopelekea wananchi kujichagulia mahali pakufanya shughuli za maendeleo bila utaratibu.

Kwa upande wa Kilimo, alieleza kuwa hali ya chakula ni ya wastani na kumekuwa na magonjwa kwa zao la mgomba ambapo takribani ekari 6.8 zimeathirika. Aidha, alieleza kuwa wakulima wamevutiwa na upandaji wa zao la parachichi

Pia, alieleza kwa upande wa hali ya mifugo ni nzuri na malisho ni mengi hakuna kituo kinachotoa huduma ya uhamilishaji. Chanjo ya mifugo haikufanyika kutoptana na ukosefu wa vitendea kazi na ugonjwa wa kichaa cha mbwa upo ila hakuna tukio lolote lililojitekeza.

Alieleza kuwa taarifa za Mapato na Matumizi zilisomwa kwenye mikutano mikuu ya vijiji. Alifafanua kuwa mapato yaliyokusanya yatokanayo na Halmashauri ya Wilaya jumla ni Sh. 390,000.00 na makusanyo ya machinjio ni Sh. 137,000.00. Vilevile, alieleza makusanyo ya Halmashauri za Vijiji ni Sh. 4,031,906.05.

Kwa upande wa makusanyo ya iCHF na Papo kwa papo jumla ni Sh. 2,306,000.00. Alieleza kwa upande wa miradi ya TASAF Awamu ya III jumla ya fedha zilizopokelewa na kuwafikia Walengwa ni Sh. 7,948,000.00 katika Vijiji vya Vuchama Ndambwe, Lambo, Mfinga na Mkuu.

Vilevile alieleza, shughuli zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa jengo la utawala shule ya msingi Ndambwe, ujenzi wa barabara Mkuu hadi Burenii na ujenzi wa barabara ya Mshesi hadi Kwarengeta. Pia, kuna ukarabati wa uwanja wa shule ya msingi Ndambwe na kijiji cha Mkuu kuna ujenzi wa Ofisi ya Kijiji. Alieleza, kijiji cha Mkuu kuna ujenzi wa shimo la taka ngumu, zahanati ya Mfinga na kufukua mifereji barabara ya Sachi.

Kwa kijiji cha Lambo kuna umalizaji wa uchimbaji wa mitaro, shule ya msingi Lambo kuna uchimbaji wa choo na zahanati ya Lambo kuna ufunikaji wa shimo la choo. Kuna ukarabati wa vyumba 2 vya madarasa na Ofisi 2 shule ya msingi Mombea.

Kwa upande wa kijiji cha Ibaya, shule ya sekondari Kilobeni kuna uchimbaji wa kiwanja na kwa shule ya sekondari Ngolea kuna ukamilishaji wa ujenzi wa darasa na msaada wa Hlamshauri unahitajika ili kukamilisha ujenzi huo.

KATA YA TOLOHA

Mheshimiwa Diwani aliwasilisha taarifa. Alieleza kwamba vikao vya kisheria vilifanyika baadhi, hali ya ulinzi na usalama si shwari kwa sababu kuna makundi makubwa ya tembo yaliyotishia usalama kwa wananchi na kuharibu mazao. Alieleza, hakuna tukio la uhamiaji haramu uliotolewa taarifa. Kilimo kinaendelea vizuri na wakulima wanajitahidi kuandaa mashamba kwa ajili ya msimu wa yuli na wameshauriwa kuhifadhi chakula.

Alifafanua kuwa barabara ya Kwakoa hadi Toloha, Kwakoa hadi Kijiji cha SimKizungo na Toloha hadi Karamba Ndea hazipitiki na zinahitaji matengenezo. Pia kuna makalvati 6 na ufukiaji mashimo katika sehemu korofii.

Kwa upande wa miundombinu, barabara ya Kwakoa – Toloha, Karamba Ndea na Mgagao zote hazipitiki zinahitaji matengenezo, hasa kipindi cha mvua maji hayatoki na makalvati yanahitajika ili maji yasituame eneo moja, hali inayosababisha ubovu wa barabara kuongezeka. Aidha, mapato ya Halmashauri ya Wilaya ni Sh. 19,656,000.00 na Halmashauri ya Vijiji ni Sh. 4,268,000.00.

Wajumbe walihoji kuwa kwanini wananchi wa Toloha wanaleta mgogoro kwa kuzuia ujenzi wa ofisi ya kudhibitiwawindajiharamunawanyamapori. Mjumbe alifafanuakuwa Wafadhilihaohawakufuatautaratibuwa ardhindimaanawananchiwanalala mikanakuzuiaujenzihuo. Aidha, Mkuuwa Wilaya ameshafanya ziarakwenye Kata ya Tolohana ameshaagizaujenzihuo uendelee.

## KATA YA CHOMVU

Mheshimiwa Diwani aliwasilisha taarifa kwa Wajumbe. Alieleza kwamba hali ya ulinzi na usalama haikuwa shwari kwa sababu kuna uhalifu uliojitokeza na watuhumiwa walionywa na kamati ya ulinzi na usalama ya Kijiji. Alieleza kuwa uhamiaji haramu na migogoro ya wafugaji na wakulima haikuwepo. Aidha, mgogoro wa ardhi umepokelewa kwenye Baraza la Kata. Alifanua kuwa vikao vya kisheria vilifanyika baadhi. Vilevile, alieleza uhamiaji haramu na migogoro ya wafugaji na wakulima hakuna. Pia alieleza kuwa, vikao vya kisheria na mikutano mikuu ilifanyika baadhi.

Alieleza Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa iCHF umekusanya jumla ya Sh. 2,760,000.00 kutoka Zahanati ya Ndorwe, Mshewa, Kimbale na Chomvu. Alieleza mapato ya papo kwa papo zilikusanywa Sh. 90,000.00 na mapato ya Halmashauri ya Kijiji yaliyokusanywa ni Sh. 1,474,550.00.

Alieleza kuwa, Chama cha Ushirika cha Ndurumo SACCOS kimekusanya madeni kwa wadaiwa sugu jumla ya Sh. 4,080,950.00 na madeni ambayo bado yanadaiwa ni Sh. 44,603,950.00. Kitengo cha Ushirika kimeombwa kusaidia kuwahamasisha wadeni hao walipe.

Shughuli za kilimo; wakulima wameendelea kupatiwa ushauri wa kuhifadhi mavuno na wamehamasishwa kulima zao la kahawa na eneo la kitalu la zao hilo limepatikana Lomwe Sekondari..

Kwa elimu msingi, mitihani ya darasa la saba ilifanyika na hakuna dosari yoyote ilijoikeza.Kuna ujenzi wa vyumba 4 vya madarasa vyenye ufa na wananchi wameendelea kuchangia.Katika maendeleo ya Jamii fedha za walengwa za TASAF zilizopokelewa jumla Sh. 7,368,000 kwa vijiji vya Mshewa, Chomvu na Kimbale.Aidha, alieleza kuwa kuna ujenzi wa Ofisi ya Kata unaoendelea.

### **KATA YA MGAGAO**

Mheshimiwa Diwani aliwasilisha taarifa. Alieleza kwamba suala la ulinzi na usalama hapakuwa shwari kwa sababu mama mmoja aliuawa na mme wake kwa kumkata kwa panga, mtuhumiwa alikamatwa.

Alieleza vikao vyote vya kisheria vilifanyika. Kwa taarifa za kisekta, upande wa elimu, kuna ujenzi wa vyumba 2 vya Maabara japokuwa michango imesimama, ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa shule ya msingi Kauzeni, na mradi huu umekamilika.

Kwa upande wa ukarabati wa mnada wa mifugo Mgagao, katika eneo la zizi la mifugo ukarabati bado haujaanza na ujenzi wa uzio wa mnada wa mifugo sehemu ya ukarabati wa uzio imekamilika.

Aidha, ushauri kwa wakulima umetolewa kuhusu kilimo bora. Kwa upande wa mifugo huduma za tiba, chanjo na ushauri kwa baadhi ya wafugaji zimetolewa na Maafisa Ugani. Pia, kwa upande wa Maendeleo ya Jamii, Idara ilitoa mafunzo ya Ujasiriamali kwa vikundi vya Vikoba.Aidha, alieleza hali ya elimu katika Kata ni ya kuridhisha.Alieleza kuwa mapato yaliyopatikana na Viji vya Mgagao ni Sh. 2,113.500 na mapato ya Halmashauri ya Wilaya ni Sh. 1,831,500.00 katika Kijiji cha Mgagao.

### **KATA YA KILEO**

Mheshimiwa Diwani aliwasilisha taarifa. Alieleza hali ya ulinzi na usalama ilikuwa shwari, Vilevile, vikao vya Kisheria vilifanyika baadhi.

Pia kwa upande wa elimu ufaulu wa mitihani kidato cha sita ulikuwa ni asilimia 100 na darasa la saba ufaulu ni asilimia 80 na wanafunzi wamefanikiwa kula chakula cha mchana, Vilevile, kwa upande wa afya hapakutokea milipuko ya magonjwa, ukaguzi wa usafi wa mazingira wanachi walihamasishwa kujenga vyoo, wanawake na wanaume walipewa elimu ya uzaziwa mpango na uhamasishaji wa kujiunga na iCHF. Makusanyo ya TFDA ni Sh. 350,000/=. Kwa upande wa mifugo, ukaguzi wa nyama ulifanyika, ushauri kwa mifugo naulishaji bora wa ng'ombe ultolewa na chanjo kku pialitolewa

Alifafanua kwa upande wa kilimo, wananchi wamesisitizwa kuandaa msahamba kwa ajili ya mvua na kuhifadhi vyakula katika maghala. Aidha, alieleza mapato ya Halmashauri ya Wilaya ikiwa ni ukaguzi na usafi wa nyama ni Sh. 280,000.00.

### **KATA YA LEMBENI**

Mhe. Diwani Alieleza kuwa hali ya ulinzi na usalama ni ya kuridhisha. Alifafanua kuwa migogoro ya mipaka ya Vijiji ilijadiliwa na Viongozi wa Vitongoji, Vijiji na Maafisa Ardhi ili kupanga namna ya kuhakiki mipaka. Alieleza kuwa vikao vya kisheria na Mikutano Mikuu ilifanyika.

Alifafanua kuwa shughuli zilizofanyika ni ujenzi wa kituo cha afya Kisangara ambapo kwa sasa mradi upo katika hatua ya umaliziaji na bado miundombinu ya maji na umeme.

Kwa upande wa elimu kuna mradi wa ujenzi wa matundu 12 ya vyoo shule ya msingi Kaili na ujenzi umefikia hatua ya umaliziaji. Pia, kuna ujenzi wa matundu 16 ya vyoo shule ya msingi Chanjale na imefikia hatua ya linta. Kuna ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa shule ya msingi Kiruru na mradi upo katika uchimbaji wa msingi na mhandisi wa ujenzi (W) anahitajika kutoa ushauri wa ujenzi. Alieleza, ujenzi wa hostel ya wasichana Kisangara sekondari, msingi umechimbwa. Alieleza kuwa, kamati za maendeleo ya Kata zinaomba Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) irejeshe asilimi 100 na asilimi 20 ambazo hazijarejeshwa kwa muda mrefu.

Alifafanua kuwa wananchi wamehimizwa kujiunga na mfuko wa Bima ya afya iCHF na waliojiunga na mfuko ni 52. Suala la usafi wa mazingira linatekelezwa kwa kila mwisho wa mwezi kama ilivyoagizwa.

Kwa upande wa Kilimo wakulima 184 walishauriwa juu ya uhifadhi wa chakula na maandalizi ya mashamba kwa ajili ya msimu wa vuli. Ushauri kwa wafugaji na matibabu ultolewa na hapakuwa na magonjwa ya milipuko kwa mifugo.

Alieleza mapato ya Halmashauri ya Wilaya yaliyopatikana ni Sh. 486,500.00 na mapato ya Halmashauri za Vijiji ni Sh. 1,745,500.00.

Baada ya taarifa kuwasilishwa ilipokelewa na wajumbe wakahoji suala la mifugo inayopitishwa kwenye barabara kuwa wanadhibiti kwa njia ipi. Wajumbe waliagiza kuwa Mkurugenzi Mtendaji (W) ahakikishe anaweka alama za vivuko vya mifugo na mifugo isipitishwe kandokando ya barabara.

Pia, walijadili kuwa majengo mengi ya shule za msingi na sekondari kwa Wilaya ya Mwanga yanahitaji ukarabati. Baada ya majadiliano, wajumbe walimuagiza Mkurugenzi Mtendaji (W) aandae bajeti ya mwaka 2018/2019 kwa ajili ya ukarabati wa majengo kwa shule zote za msingi na sekondari.

### **KATA YA KIRYA**

Mheshimiwa Diwani aliwasilisha taarifa. Alieleza kwamba suala la ulinzi na usalama ni ya wastani. Migogoro ya wakulima na wafugaji inaendelea kutatuliwa kwa njia ya vikao. Aidha, alieleza kuwa mikutano mikuu na vikao vya kisheria vilifanyika.

Kwa upande wa mifugo, hali ya mifugo ilikuwa ni nzuri na milipuko ya magonjwa kwa mifugo hakuna.

Shughuli zilizofanyika ni pamoja na kutoa ushauri, ukaguzi wa nyama, kukusanya ushuru wa ukaguzi wa nyama na nyumba za biashara, kutembelea wafugaji na utoaji wa elimu ya ufugaji bora na wenye tija, utoaji wa tiba na ukusanyaji wa takwimu mbalimbali za mifugo.

Aidha alieleza, ujenzi wa makambi mawili kijiji cha Njia Panda, umekamilika ila bado ukamilishaji wa vyoo viwili. Alieleza kuna ujenzi wa vyumba vinne shule ya msingi Kiti cha Mungu, ila vyumba viwili vimekamilika na bado vyumba viwili.

Alieleza mapato ya Halmashauri ya Vijiji ni Sh 4,956,000.00 na Mapato ya Halmashauri ya Wilaya ambayo yanatokana na ushuru wa mazao ni jumla Sh. 5,810,400.00. Pia makusanyo ya bima ya afya iliyoboreshwa iCHF ni Sh. 1,440,000.00.

### **KATA YA KIVISINI**

Mheshimiwa Diwani aliwasilisha taarifa na alieleza kwamba hali ya ulinzi na usalama ni nzuri. Mahusiano kati ya wakulima na wafugaji ni mazuri. Alieleza kuwa vikao vya kisheria vilifanyika baadhi.

Shughuli zilizofanyika ni jitihada za kupambana na uharibifu wa mazingira na kukemea biashara haramu ya usafirishaji wa mkaa. Vilevile, elimu imekuwa ikitolewa kuhusu uhifadhi wa mazingira kwa wananchi.

Alieleza mapato ya ndani katika Kata kwenye vyanzo vya mapato ya Halmashauri ya Wilaya ni Sh. 60,000.00 na Mapato ya Halmashauri ya Kijiji cha Kwanyange umekusanywa ushuru wa jumla ya Sh. 8,020,000.00, Kijiji cha Kitoghoti mapato ni Sh. 1,465,300.00 na Kijiji cha Kivisini imekusanywa jumla ya 400,000.00, ambapo jumla kuu ni Sh. 9,885,300.00.

Pia, alieleza kuwa, kuna ujenzi wa nyumba ya watumishi na ujenzi wa Placentor na Incenerator kwenye zahanati ya Kivisini. Kwa shule ya msingi Kivisini kuna ujenzi wa choo unaoendelea. Kwa Kijiji cha Kwanyange kuna ukarabati wa kisima cha maji na ujenzi wa choo shule ya msingi Kwanyange. Alieleza elimu imetolewa juu ya upimaji wa Afya ili kujitambua iwapo umeambukizwa na VVU kwa wajawazito na wenza wao imetolewa. Alisema mfuko wa afya ya jamii ulioboreshwa iCHF mapato yaliyokusanywa ni Sh. 330,000.00.

Kwa upande wa kilimo, wakulima walishauriwa kuvuna chakula na uhifadhi wa chakula. Kwa upande wa mifugo wafugaji walishauriwa kuhusu ufugaji bora na matibabu kwa mifugo. Pia, alifafanua shughuli za maendeleo ya jamii zilizotekelizwa ni uwekaji na ukopaji wa vikundi mbalimbali na ufuutiliaji wa vikundi vikiwemo wanawake na vijana.

Kwa upande wa mradi wa maji, kuna kisima cha Kwanyange kilifanyiwa ukarabati ili wananchi waweze kupata maji kwa urahisi.

## **KATA YA KIGHARE**

Mheshimiwa Diwani aliwasilisha taarifa. Alieleza kuwa hali ya ulinzi na usalama si shwari kwa sababu kulitokea matukio ya wizi wa mifugo, mazao na biashara ndogondogo. Aidha, vikao vya kisheria vilifanyika. Alieleza usafi wa mazingira kila mwisho wa mwezi ulifanyika.

Alieleza kuwa Mapato ya Halmashauri kwa upande wa ushuru wa nyama na mapato ya leseni ni Sh. 249,000.00 na Mapato ya upigaji chapa ng'ombe ni Sh. 166,000.00.

Alieleza mapato ya papo kwa papo kwenye Hospitali ya Usangi ni Sh. 7,274,000.00. Alieleza kwa Zahanati ya Usangi, Kighare na Ndanda mapato yao ni Sh. 6,073,540.00. Kwa upande wa miradi ya maendeleo, hali ya miundombinu ya madarasa siyo nzuri na inahatarisha usalama wa wanafunzi, kuna ujenzi wa jengo la utawala ambapo lipo kwenye hatua ya umaliziaji.

Kwa upande kilimo. Chakula kipo cha kutosha, pia kuna uhamasishaji wa mazao ya biashara kama kahawa na maparachichi ya muda mfupi. Alieleza usambazaji wa maji unaendelea vizuri kwa kusimamiwa na Jumuiya za watumia maji zilizopo.

Vilevile, barabara zimekuwa hazipitiki na marekebisho madogomadogo yamekuwa yakifanyika kwa msaragambo na maeneo mengi yamefanyiwa ukarabati na TARURA.

Kwa upande wa mazingira, udhibiti wa ukataji wa miti na uchomaji wa mkaa umeimarishwa na wananchi wameendelea kuhamasishwa kutunza mazingira.

Baada ya taarifa kuwasilishwa, ilipokelewa na Wajumbe wakahoji na kujadili suala la vijana wanaoshindwa kufanya kazi za kijamii hasa wakati wa kazi, kwa kujihusisha na ulevi. Wajumbe walimuagiza Mkurugenzi Mtendaji (W) ahakikishe kuwa utoaji wa leseni za vimeo kwa Wilaya ya Mwanga unazingatia udhibiti wa uuzaji wa pombe wakati wa kazi.

### **KATA YA KIFULA**

Mheshimiwa Diwani aliwasilisha taarifa. Alieleza kuwa hali ya ulinzi na usalama ni nzuri kwa sababu hakuna tukio la kuhtarisha amani lililojitekeza.

Alieleza kuwa, vikao na mikutano mikuu pamoja na WDC vilifanyika. Pia, taarifa za mapato na matumizi zilisomwa kwenye Mikutano Mikuu ya Vijiji. Aidha, vikao vyta kisheria vilifanyika.

Alieleza kuwa kuna ujenzi wa vyoo vyta wanafunzi unaoendelea shule ya msingi Rangaa na Fumbua Ng'ombe. Alifafanua ujenzi wa madarasa shule ya msingi Kifula unaendelea.

Pia, wakulima wamehamasishwa kununua miche ya maparachichi, kuanzisha shamba la mfano katika ushirika wa Kifula nauhamasishaji wa upandaji wa migomba.

Kwa upande wa miradi ya maendeleo, ujenzi wa ofisi ya kijiji cha Kadengere unaendelea na umefikia hatua ya upauzi, Zahanati ya Rangaa ujenzi unaendelea na umefikia hatua ya kumwaga jamvi, ujenzi wa kiwanda cha matofali na nyumba za watumishi Raa zinaendelea kujengwa. Pia, kuna ujenzi wa zahanati Kijiji cha Masumbeni ambao umekwama kwa sababu ya ukosefu wa fedha na ofisi ya kata haijakamilika nayo inahitaji fedha ili ikamilike.

Vilevile, kuna uanzishwaji wa mradi wa usafi wa majumbani, ujenzi wa vichanja, uchimbaji wa mashimo ya taka naujenzi wa vyoo vyta kisasa majumbani na wananchi wameshiriki usafi wa mwisho wa mwezi.

Alieleza kuwa mapato ya ukaguzi wa nyama ni Sh.192,000.00 na ushuru wa soko Kijiji cha Kisanjuni na Halmashauri ya Wilaya ni Sh. 14,382,471.00 na ada ya leseni ni Sh. 261,000.00. Kwa upande wa makusanyo ya papo kwa papo ni Sh. 2,000,000 na michango ya iCHF makusanyo ni Sh. 1,353,333.33.

### **KATA YA KIRONGWE**

Mheshimiwa Diwani aliwasilisha taarifa na alieleza kwamba, vikao vyta kisheria vilifanyika. Alieleza hali ya usalama haikuwa nzuri kwa sababu kulikuwa na matukio machache ya uhalifu yalijiyo jitokeza na kushughulikiwa katika ngazi ya Vitongoji, Vijiji na Kata.

Alieleza kuwa hali ya chakula haikuwa nzuri kwa sababu mvua za msimu wa Vuli kuwa kidogo na kusababisha upungufu na mfumuko wa bei ya vyakula.Pia, alieleza Mikutano Mikuu na vikao vyta Kisheria yote ilifanyika.

Kwa upande wa elimu, taaluma inaendelea vizuri lakini kuna upungufu wa walimu kwenye shule za Msingi na Sekondari, kuna uchakavu wa madarasa, wanafunzi wameanza kula chakula cha mchana shulenii. Kwa upande wa kilimo na ushirika, ushauri ultolewa kwa wakulima, kuwa kuna uanzishwaji wa vitalu vya miche kwa wakulima wa zao la kahawa.

Aidha, kwa upande wa mapato ya uchinjaji wa Kondoo na ng'ombe kilipatikana kiasi cha Sh. 241,600.00.

Alielea kuwa, ujenzi wa ofisi ya kijiji cha Vuagha na Kijiji cha Mwero yote imefikia hatua ya ujenzi wa msingi, inasubiriwa kukaguliwa na Mhandisi wa Ujenzi (W). Pia kuna mradi wa ujenzi wa ukumbi wa mkutano ambao haujakamilika na kuna mbaao 50 na bati 33 ambazo zilitolewa na Mheshimiwa Mbunge. Huduma ya watumia maji aliyekuwa mgawia maji amejiuzulu kwa sababu ya kutokulipwa posho ya kutosha.

Vilevile, alielea kuwa miundombinu inafanyiwa ukarabati kwa njia ya msaragambo. Alielea kuwa kuna uchimbaji na ukarabati kwa njia ya msaragambo kwenye barabara za Mbore, Kiriche, Lomwe na Vuagha.

Alielea, mapato ya Halmashauri ya Vijiji yaliyopatikana ni Sh. 802,500.00. Alielea kwa upande miradi ya TASAF Awamu ya III jumla ya fedha zilizopokelewa na kuwafikia walengwa ni Sh.3,723,000.00 kwa vijiji vya Lomwe, Vuagha, Kiriche na Mbore. Aidha, alifafanua kuwa, jumuiya za watumia maji kijiji cha Lomwe ni Sh. 1,137,498.30.

### **KATA YA MWANIKO**

Mheshimiwa Diwani aliwasilisha taarifa. Alielea kwamba hali ya ulinzi na usalama inaridhisha. Aidha, vikao vya kisheria ikiwemo Halmashauri ya Vijiji na mkutano mkuu vilifanyika. Vilevile, alielea usafi wa mazingira unafanyika vizuri na ulinzi wa vyanzo vya maji umeimarishwa na wananchi wameendelea kuhamasishwa kutunza mazingira.

Alielea kuwa makusanyo ya fedha za iCHF yaliyopatikana kiasi cha Sh. 2,880,000.00 kwa Zahanati za Mriti, Mwaniko, Vuchama Ngofi na Mangio. Kwa upande wa Papo kwa papo ni Sh. 132,000.00. Mapato yaliyopatikana kutokana na ukaguzi wa nyama ni 124,000.00

Shughuli zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa Zahanati ya Kata ya Mwaniko ambapo mradi bado unaendelea na wafadhili wamekamilisha msingi wa mzunguko wa nje na ndani, hatua iliyofikiwani uwekaji wa jamvi. Alielea mradi wa Kituo cha afya Mangio bado unaendelea na mabati yaliyoombwa yanakumbushiwa msaada kwa Mkurugenzi Mtendaji (W) ili kuezeka vyumba 11.

Alieleza kuwa Zahanati ya Mangio inakabiliwa na upungufu wa watumishi, uchakavu wa majengo na sehemu maalumu ya kuteketeza taka. Vilevile, alieleza kuwa nyumba ya watumishi Zahanati ya Mriti na Mangio haina shimo la kutupia kondo la nyuma.

Mradi wa ukarabati kwenye Zahanati ya Vuchama na tathmini imeshafanyika, fedha inaombwa kutoka Halmashauri ili kukamilisha mradi huo.

Pia, mradi wa Ofisi ya Kijiji cha Mriti umekamilika kwa asilimia 85, kiasi cha fedha kinachohitajika ni Sh. 3,476,000. Ili kukamilisha mradi. Mradi wa Ofisi ya Kijiji cha Mwaniko ambao unajengwa kwa ruzuku na nguvu za wananchi bado haujakamilika na fedha inayohitajika ni Sh. 2,700,000.00. Vilevile, hali ya chakula katika Kata ya Mwaniko ni nzuri.

Kwa upande wa mazingira, suala la usafi na mazingira unafanyika kwa utaratibu uliowekwa na kila mwisho wa mwezi usafi unafanyika. Kwa upande wa hali ya chakula imeimarika kwakuwa mvua za masika ni nyingi za kutosha.

Kwa upande wa mradi wa maji wa uchimbaji wa visima vikubwa kwa vijiji vya Mwaniko, upimaji wa maeneo yenye maji ulishafanyika na sasa timu ya tathmini inasubiriwa kwa ajili ya usambazaji wa maji hayo. Alieleza kwa vijiji vya Mriti na Mangio upimaji ulishafanyika lakini uchimbaji bado haujaanza.

Kwa upande wa elimu ya msingi, shule ya msingi Chimbii hawana nyumba ya mwalimu, shule ya msingi Mriti inakabiliwa na changamoto ya choo cha walimu na ujenzi umeshaanza kwa kutumia nguvu za wananchi. Pia, shule ya msingi Mangio chumba cha darasa la awali kimeshajengwa kwa asilimia 70 na nyumba za walimu zinakabiliwa na tatizola umeme, shule ya msingi Njuweni na Managugu ina ukosefu wa darasa la awali. Wananchi wameanza kuchangia ujenzi wa madarasa ya awali. Pia, Vuchama haina Mwalimu wa darasa la awali. Pia, shule ya msingi Mcheni inakabiliwa na uchakavu wa mabati, ofisi ya walimu na baadhi ya madarasa.

Aidha, kwa upande wa elimu ya sekondari kuna uhaba wa mwalimu shule ya Sekondari Chaangaja, maabara 2 hazijakamilika, shule inakabiliwa na uchakavu wa madarasa, ujenzi wa ngazi unahitajika katika maeneo mbalimbali ya shulenii. Alieleza kuwa shule ya sekondari Ubang'i, nyumba ya mwalimu inaendelea kujengwa kwa sababu imepata Wafadhili wa Taasisiya Elimu Tanzania. Alieleza kuwa, kutokana na jiografia ya eneo la shule ya sekondari Changaaja, inatakiwa zijengwe ngazi katika maeneo mbalimbali ya shule ili kuepusha ajali.

Chakula cha mchana shulenii bado ni changamoto kwani ni asilimia 30 tu ya wanafunzi ndio wanaopata chakula cha mchana shulenii.

## **KATA YA KILOMENI**

Mheshimiwa Diwani aliwasilisha taarifa. Alieleza kwamba hali ya ulinzi na usalama ni nzuri kiasi kwa sababu kuna matukio madogo madogo yaliyojitokeza lakini yalitatuliwa. Vikao vya kisheria vilifanyika.

Alieleza, kuna matengenezo ya barabara ya Mseko – Kilomeni – Kwakoa na barabara ya Kilomeni – Kisekibaha wananchi wameendelea nauchimbaji wa barabara.

Kuna ujenzi wa vyoo shule za msingi Kilomeni mbapo gharama za mradi hazijapatikana na Idara ya ujenzi inahitaji kuandaa BOQ na katika shule ya msingi Shighati Idara ya ujenzi inatakiwa kutoa huduma ili choo kiendelee kujengwa.

Kwa shule ya sekondari Maghare, upauaji umekamilika bado uwekaji wa mabati. Alieleza Kijiji cha Sofe shule ya msingi Shighati kuna darasa 1 ambapo upo katiaka hatua ya umaliziaji wa ukuta.

Ujenzi wa bwalo la chakula shule ya msingi Sofe, hatua iliyofikiwa ni uwekaji wa mabati. Kwa mradi wa maji vijiji vyote vya Kata ya Kilomeni, miradi yote ipo katika hatua za matazamio.

Vilevile, zahanati ya kwa Msonge Sofe, kuna ujenzi wa vyumba viwili ambapo nguvu za wananchi zinahitajika ili mradi uendelee.

Kwa upande wa kilimo. hali ya chakula inaridhisha. Ushauri na matibabu kwa mifugo ulitolewa. Alieleza usafi wa mazingira wa mwisho wa mwezi ulifanyika. Aidha, alieleza kuwa utunzaji wa msitu wa Kindoroko unaendelea kufuatiliwa.

Mratibu wa Dawati la Uwezeshaji wananchi Kiuchumi aliwasilisha majumuishao ya vijiji vyote na ushauri ulipokelewa na wananchi. Wananchi waliomba huduma ya umeme wa REA ili umeme huo uweze kuwasaidiakwenye shughuli zao za kila siku. Idara ya maendeleo ya jamii imeendelea kuhamasisha wananchi kuhusu shughuli mbalimbali zinazohusu maendeleo.

Aidha, alieleza kuwa, mapato ya Halmashauri ya Wilaya yaliyokusanywa ni Sh. 76,000.00. na mapato ya Halmshauri ya Kijiji yaliyokusanywani Sh. 832,350.00 na papo kwa papo pamoja na iCHF haikukusanywa kwa sababu hajakaa vizuri.